**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**MAHKAMA**

# MUONGOZO WA JAJI MKUU NAMBARI 1 WA 2026
# MUONGOZO WA MATUMIZI YA MFUMO WA KIELETRONIKI WA USIMAMIZI WA MASHAURI (e-CMS)

1. Mahkama ya Zanzibar inaendelea kuboresha utoaji wa huduma zake kupitia matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza uwazi, ufanisi na upatikanaji wa haki. Maboresho hayo ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa kieletroniki wa usimamizi wa mashauri (Electronic Case Management System – eCMS) utakaonza kutumika rasmi katika Mahkama za kawaida na Mahkama za Kadhi kuanzia tarehe 01 Julai, 2026. Usimamizi wa mashauri unajumuisha ufunguaji wa kesi, usajili, usikilizwaji na utoaji wa maamuzi ya Mahkama.

2. Ili kuhakikisha mabadiliko ya kutoka analogia kwenda kidigitali yanafanyika kwa ubora na ufanisi mkubwa mfumo huo utaanza kutumika kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza itaanza tarehe 01 Julai, 2026 na itahusisha Mahkama Kuu Masjala Kuu Tunguu pamoja na Divisheni zake, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa Tunguu na Mahkama zote zilizopo Mkoa wa Mjini Magharibi.

3. Awamu ya pili itaanza tarehe 01 Agosti, 2026 na itahusisha Mahkama zote zilizopo Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Mkoa wa Kusini Unguja.

4. Awamu ya tatu itaanza tarehe 01 Septemba, 2026 na itahusisha Mahkama Kuu Masjala Ndogo ya Pemba, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa Pemba, pamoja na Mahkama zote zilizopo Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkoa wa Kusini Pemba.

5. Mashauri yatakayoanza kufunguliwa na kusikilizwa katika mfumo wa kieletroniki kwa kipindi hicho kilichotajwa kwa Mahkama husika, yatakuwa ni mashauri mapya tu. Kwa mashauri yaliyofunguliwa kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo yataendelea kusikilizwa kwa utaratibu wa zamani.

6. Wakati wa usikilizaji wa awali (preliminary hearing) katika mashauri ya jinai, mwenendo uliochukuliwa kieletroniki utaprintiwa na kusainiwa na wahusika na kisha kumbukumbu hizo zitaskaniwa na kupandishwa kwenye mfumo.

7. Rufaa au maombi yanayotokana na mashauri ambayo hayakufunguliwa na kusikilizwa kwa njia ya kieletroniki yataendelea kusikilizwa kwa njia ya zamani.

8. Kumbukumbu zote zitakazowasilishwa na kuhifadhiwa katika mfumo wa e-CMS zitachukuliwa kuwa ni kumbukumbu rasmi za Mahkama na zitatumika kwa madhumuni ya kiutawala na kimahkama kwa mujibu wa sheria.

9. Kutakuwa na madawati ya usaidizi (help desks) katika kila Mahkama ili kuwasaidia wananchi wasioweza kutumia mfumo.

10. Kipindi ambacho mfumo utakuwa umeanza kutumika katika Mahkama husika, hakuna shauri litakalokubaliwa kufunguliwa na kusikilizwa kwa njia ya zamani isipokuwa kwa muongozo wa Jaji Mkuu.

11. Muongozo huu utaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Jaji Mkuu na unaweza kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara kwa mujibu wa mahitaji katika kipindi cha matumizi ya mfumo.

Muongozo huu umetolewa na kusainiwa leo tarehe 26 Juni, 2026.



……………………………………

KHAMIS RAMADHAN ABDALLA

**JAJI MKUU WA ZANZIBAR**